



## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero anapenda kuwatangazia Watanzania wote kuwa amepokea Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/361/01"B"/49 cha tarehe **13 Februari, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III**. Hivyo Watanzania wote wenye Sifa mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:-

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (VILLAGE EXECUTIVE III) - NAFASI NNE (4)

#### i) *Sifa za Kitaaluma kwa Mwombaji;*

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI), aliyepata mafunzo katika ngazi ya Cheti (**NTA LEVE 5**) ambaye amehitimu mafunzo ya Astashahada / Cheti katika moja ya fani zifuatazo;\_
- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### ii) *Majukumu ya kufanya:-*

- a) Kuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- b) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- c) Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji.

- d) Kuwa Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauriya Kijiji.
  - e) Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
  - f) Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kukondoa Njaa, Umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
  - g) Kuwa Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
  - h) Kusimamia, Kukusanya na Kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
  - i) Kuwa Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalam waliopo katika Kijiji
  - j) Kupokea, Kusikiliza na Kutatua Malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
  - k) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
  - l) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- iii) **Masharti ya Ajira**  
Ajira ya Kudumu
- iv) **Mshahara**  
Ngazi iya Mshahara wa kuanzia ni **TGS.B**
- v) **Masharti ya jumla kwa waombaji**
1. Awe Raia wa Tanzania.
  2. Awe na Umri wa kuanzia miaka 18 na asizidi miaka **45**.
  3. Mwombaji lazima aambatanishe Wasifu wake Binafsi (**CV**) akionesha mawasiliano yake ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
  4. Muombaji anatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (**National Identification number**) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (**NIDA**).
  5. Mwombaji aombe kwa kuzingatia Masharti ya **TANGAZO LA KAZI**.
  6. Maombi yote yaambatane na nakala za Vyeti vya Taaluma (**Certificates**), nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) kwa wale waliofika kiwango hicho cha Elimu, Vyeti vya kuhitimu Mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia Sifa za kazi husika.



*Transcripts, Testimonials, Provisional Results, Statement of Results na Hati za matokeo ya Kidato cha IV au VI havitakubaliwa.*

7. Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishie barua yake ya Maombi ya nafasi ya kazi kwa Mwajiri wake na Mwajiri ajiridhishe ipasavyo.
8. Mwombaji aoneshe Wadhamini Wawili (2) na anuani zao na namba zao za simu.
9. Mwombaji mwenye Cheti cha Kidato cha Nne/ Sita na Cheti cha Taaluma ambacho Kimepatikana nje ya Nchi; ahakikishe kuwa Vyeti hivyo vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE).
10. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
11. Watakaochaguliwa kufanya Usaili watajulishwa tarehe ya Usaili.
12. Maombi yaambatane na picha mbili (Passport size) za hivi karibuni. Picha iandikwe jina la Mwombaji kwa nyuma.
13. Maombi yaambanishwe na nakala ya Cheti cha Kuzaliwa cha Mwombaji.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/3/3023 saa tisa na nusu (9.30) Alasili

*Maombi yote yatumwe kwa:*

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO,  
S.L.P. 663,  
MVOMERO.**

Tangazo hili limetolewa na;

*Phillipo*

Dkt. Phillipina Phillipo

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
MVOMERO**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO  
S.L.P 663, MOROGORO

/smn